**KILIMANJARO CHRISTIAN MEDICAL CENTRE (KCMC)**
***Taasisi ya Shirika la Msamaria Mwema***
**Moshi**

# TAARIFA KWA UMMA

## UCHANGIAJI WA UJENZI WA JENGO LA MATIBABU YA MOYO-KCMC

***Dar es Salaam*** ***09 Aprili, 2026***

Kilimanjaro Christian Medical Centre – KCMC ni hospitali ya Rufaa ya Kanda inayotoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi (consultant and referral specialized hospital) iliyoanzishwa tarehe 06 Machi, 1971 ikuhudumia wananchi wa Kanda ya Kaskazini ya Tanzania, inayojumuisha mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Hospitali hii ipo Mkoa wa Kilimanjaro lakini inahudumu wahitaji hata kutoka nje ya mipaka ya eneo lake la rufaa.

### Magonjwa ya Moyo Kimataifa

Magonjwa yasiyoambukiza (Non-communicable diseases – NCDs) kwa sasa yanachangia takribani asilimia 70 ya vifo duniani. Miongoni mwa magonjwa haya, magonjwa ya moyo na mishipa (cardiovascular diseases – CVDs) ndiyo chanzo kikuu cha vifo.

Magonjwa kama Kiharusi (stroke) na Ugonjwa wa kuziba kwa mishipa ya moyo (ischemic heart disease) yanachangia sehemu kubwa ya vifo hivi. Zaidi ya asilimia 78 ya vifo vinavyotokana na magonjwa yasiyoambukiza hutokea katika nchi zenye kipato cha chini na cha kati (lower and middle income). Tofauti na nchi zilizoendelea, katika nchi hizi magonjwa ya moyo huanza kuathiri watu wakiwa katika umri mdogo, hali inayopunguza nguvu kazi na kuathiri maendeleo ya kiuchumi.

### Magonjwa ya Moyo Hospitali ya KCMC

Magonjwa ya moyo ni miongoni mwa sababu kuu za wagonjwa kulazwa KCMC; takwimu za hospitali zinaonyesha kuwa, asilimia 14.4 ya wagonjwa wanaolazwa ni wagonjwa wa moyo ambapo hulazwa hospitalini kwa wastani wa siku 9 hadi 10 na asilimia 38.5 ya wagonjwa wanaoruhusiwa hulazwa tena hospitalini baada ya muda na hivyo kiwango cha vifo kwa wagonjwa wa moyo ni takribani asilimia 18.3 ya vifo vyote vinavyotokea KCMC.

Katika kipindi cha miaka mitano (2020–2025), jumla ya wagonjwa 24,585 kati ya 135,136 waliolazwa hospitalini KCMC walikuwa na magonjwa ya moyo. Aidha, zaidi ya wagonjwa 133,000 kati ya 1,502,236 wa nje walipatiwa huduma za matibabu ya moyo katika kipindi hicho, hii ni ishara ya ongezeko kubwa la magonjwa ya moyo nchini Tanzania kwa miaka ya hivi karibuni.

### Lengo Kuu la Mradi

Katika kukabiliana na ongezeko la magonjwa ya moyo nchini na kuboresha huduma za kibingwa, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini – KCMC imeanzisha mpango maalum unaojumuisha wazo la kuboresha huduma za moyo, ujenzi wa miundombinu ya kisasa pamoja na kuimarisha kliniki ya moyo.

Kuanzisha Kituo cha kisasa cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa (fully functional Cardiovascular Centre) katika hospitali ya KCMC kitakachotoa huduma kamili za uchunguzi, matibabu na ufuatiliaji wa wagonjwa wa moyo kwa Kanda ya Kaskazini ya Tanzania na maeneo mengine ndani na nje ya nchi.

**Malengo Mahususi**

Kuimarisha kinga, kutoa elimu kwa jamii na uchunguzi wa mapema wa magonjwa ya moyo, Kuanzisha huduma za kisasa za uchunguzi na matibabu ya moyo, Kutoa matibabu ya dawa, matibabu ya kutumia mirija maalum (catheter-based treatment), upasuaji wa moyo (cardiac surgery), Kutoa huduma za urekebishaji wa afya ya moyo (cardiac rehabilitation) pamoja na Ufuatiliaji wa muda mrefu na huduma za kupunguza maumivu (palliative care). Faida ni kupunguza uhitaji warufaa za nje ya nchi pia kupunguza mzigo kwa taasisi pekee iliyoko Tanzania mpaka sasa. Kuwa jukumu la Afya sio la Serikali tu. Hiyo ndo maana KCMC inataka kuanza huduma hii.

**Ujenzi wa Jengo**

Kitengo hiki kitakapokamilika kitakuwa na jengo la kisasa lenye ghorofa tatu litakalojumuisha:

- Vyumba viwili (2) vya upasuaji wa moyo (cardiac surgery theatre)
- Maabara mbili (2) za uchunguzi wa mishipa ya moyo (catheterization laboratory)
- Vyumba vya wagonjwa mahututi (Intensive Care Unit – ICU) kwa watu wazima na watoto
- Vitengo vya uangalizi maalum baada ya ICU (step-down ICU units)
- Vitanda 102 vya wagonjwa wa ndani
- Kliniki za wagonjwa wa nje
- Kitengo cha urekebishaji wa afya ya moyo (cardiac rehabilitation unit), Maabara za uchunguzi na huduma za dawa.

**Gharama za Mradi**

**Ujenzi wa jengo: Utagharimu shilingi bilioni 25 za Kitanzania na Vifaa tiba na vifaa vya hospitali vitagharimu jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 25 za Kitanzania**

Aidha, wataalamu watakaohudumia kitengo hiki wanapata mafunzo yao nchini India na Tanzania na wanapata ufadhiliwa kutoka kwa mdau aitwae Global Heartcare Foundation

**Upatikanaji fedha na Ushirikiano wa Kimataifa**

KCMC tayari imeingia makubaliano ya ushirikiano na wadau wa kimataifa ambao wamekubali kufadhili asilimia 90 ya gharama za ujenzi.

**Rai kwa watanzania wote (ndani na nje ya nchi)**

Kupitia vyombo vya habari, tunatoa wito wa dhati kwa Watanzania wote popote mlipo ndani ya mipaka ya nchi yetu na nje ya nchi kuungana katika juhudi hii ya kitaifa.

Huu si mradi wa KCMC pekee. Huu ni mradi wa Watanzania wote. Ni mradi wa kulinda maisha ya ndugu zetu, wazazi wetu, watoto wetu, na vizazi vijavyo.

Tunawaomba Watanzania wa kila rika na kila nafasi vijana, wazee, wafanyabiashara, wafanyakazi, wakulima, viongozi, na diaspora yetu kuchangia kwa moyo wa uzalendo na mshikamano.

Kila mchango ni muhimu. Kila mchango ni uhai. Kila mchango ni tumaini.

Kwa pamoja, tunaweza kujenga kituo hiki.

Kwa pamoja, tunaweza kuokoa maisha.

Na kwa pamoja, tunaweza kuandika historia mpya ya huduma za afya nchini Tanzania.

**JINSI YA KUCHANGIA**

Ndugu Watanzania, Unaweza kuchangia kupitia njia zifuatazo:

**AKAUNTI JINA: KCMC MOYO**

- Bank of Africa – 04563580007
- CRDB Bank – 0150686858800
- NMB Bank – 40310194610
- NBC Bank – 017172000770

MITANDAO YA SIMU:

- Mixx by Yas – 15175376
- Halotel (Halopesa) – 23758475

Aidha, kwa wale watakaopenda kutoa michango yao ana kwa ana, mnakaribishwa kufika moja kwa moja katika Hospitali ya KCMC, Moshi, ambapo tutawapokea kwa heshima na kuwapa ushirikiano unaostahili.

RAI KWA WATANZANIA WOTE (NDANI NA NJE YA NCHI)

**Tuchangie leo. Tuokoe maisha kesho.**
**Asanteni kwa kunisikiliza.**

**Imetolewa na;**

**Uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini-KCMC**

**09 Aprili 2026**